**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# MKUTANO WA SITA

# YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI

**10 FEBRUARI, 2017**

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI
## TAREHE 10 FEBRUARI, 2017

## I. DUA:

Saa 3.00 Asubuhi Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mwenyekiti) alisoma Dua na kuongoza kikao.

**Makatibu Mezani**: Lawrence Makigi
Charles Mloka
Lina Kitosi

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani:-

i. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) aliwasilisha Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2013/14 – 2014/15;

ii. Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Taarifa ya Serikali kuhusu majibu ya Serikali juu ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*) kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2015;

iii. Waziri wa Elimu, Sayansi,Tekinolojia Mafunzo ya Ufundi aliwasilisha Taarifa zifuatazo:-

   a) Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa na Chuo Kikuu cha Ardhi kwa Mwaka wa Fedha 2014/15 *(The Annual Report and audited Accounts of Ardhi University for the Financial Year 2014/2015);*

   b) Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Chuo Kikuu Mzumbe kwa mwaka wa Fedha ulioishia terehe 30 Juni, 2015 *(The Annual Report and Audited Accounts of Mzumbe University for the Financial Year ended 30th June, 2015).*

iv. Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano aliwasilisha Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 *(The Annual Report and Audited Accounts of Road Fund Board fo Financial Year 2012/2013);*

v. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo aliwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017;

vi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge aliwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017;

vii. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama aliwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

## III. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na. 105: Mhe. Ally Seif Ungando

Nyongeza:

i. Mhe. Ally Seif Ungando
ii. Mhe. Abdallah Hamisi Ulenga

Swali Na. 106: Mhe. Cecilia Daniel Paresso

Nyongeza:

i. Mhe. Quambalo Willy Qulwi
ii. Mhe. Ryoba Chacha Marwa

### WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

Swali Na. 107: Mhe. Desderius John Mipata

Nyongeza:

i. Mhe. Desderius John Mipata
ii. Mhe. Cecil David Mwambe
iii. Mhe. George Malima Lubeleje

Swali Na. 108: Mhe. Abdallah Hamis Ulenga

Nyongeza:

i. Mhe. Abdallah Hamis Ulenga
ii. Mhe. Zacharia Paul Issay
iii. Mhe. Zubeir Mohammed Kuchauka

### WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Swali Na. 109: Mhe. Khadija Nassir Ali [Kny. Mhe. Mwantakaje Haji Juma]

Nyongeza:
i. Mhe. Khadija Nassir Ali
ii. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi
iii. Mhe. Salma Mohammed Mwasa

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Swali Na. 110: Mhe. Haji Khatib Kai
Nyongeza:
i. Mhe. Ally Saleh Ally
ii. Mhe. Susan Anselm Lyimo
iii. Mhe. Amina Saleh Mollel

**WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

Swali Na. 111: Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab
Nyongeza:
i. Mhe. Balozi Adadi Mohammed Rajab
ii. Mhe. Yahaya Omary Massare
iii. Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

Swali Na. 112: Mhe. Jamal Kassim Ali
Nyongeza:
i. Mhe. Jamal Kassim Ali
ii. Mhe. Frank George Mwakajoka
iii. Mhe. Shally Joseph Raymond

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Swali Na. 113: Mhe. Raphael Japhary Michael
Nyongeza: Mhe. Raphael Japhary Michael

Swali Na.114: Mhe. Daniel Edward Mtuka [kny. Mhe. Omary Ahmed Badweli]

Nyongeza: Mhe. Daniel Edward Mtuka

**WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Swali Na. 115: Mhe. Aida Joseph Khenani
Nyongeza: Mhe. Aida Joseph Khenani

Swali Na. 116: Mhe. Venance Methusalah Mwamoto
Nyongeza: Mhe. Venance Methusalah Mwamoto

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Swali Na. 117: Mhe. Sophia Mathayo Simba
Nyongeza: Sophia Mathayo Simba

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Swali Na. 118: Mhe. Leonidas Tutubert Gama
Nyongeza: Mhe. Leonidas Tutubert Gama

## IV. MATANGAZO:

- Wageni mbalimbali waliohudhuria Bungeni walitambulishwa.

- Waheshimiwa Wabunge waliopiga picha za Vitambulisho vya Taifa walijulishwa waende Ukumbi uliokuwa Dispensary wakachukue.

## V. MUSWADA WA SHERIA WA SERIKALI:

Muswada ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka, 2017. (*The Written Laws (Miscelleneous Amendments) Bill, 2017*).

**MWONGOZO WA SPIKA:**

1. Mhe. Hamidu Hassan Bobali aliomba Mwongozo chini ya Kanuni ya 68(7) kuhusu nini hasa tafsiri ya neno “ugaidi” kwani katika Maswali mbalimbali yanayoulizwa na Wabunge majibu yanayotolewa na Serikali yanakanusha kuwepo kwa matukio ya Ugaidi hapa nchini;

2. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara alitaka kujua Maazimio yaliyopitishwa tarehe 8/2/2017 kuhusu Hoja yake ya masuala yanayohusu Haki za Bunge ambapo Wabunge walijadili na kuazimia kwamba, Maazimio hayo yawapeleke wahusika kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Katika madai yake Mhe. Waitara alieleza kwamba, magazeti ya siku hiyo yametoa Taarifa kwamba Katibu wa Bunge amesema Maazimio hayo sio halali kwani hayakufuata utaratibu hivyo anaomba kupata ufafanuzi zaidi;

3. Mhe. Abdallah Ally Mtolea aliomba Mwongozo kuhusu Swali Na. 109 kwamba linafanana na Swali lililoulizwa tarehe 31/1/2017 lakini majibu yake ni tofauti. Serikali katika Swali moja ilijibu hakuna matukio yaliyofanyika Zanzibar na Serikali haina Taarifa lakini majibu ya swali jingine ni kwamba, Serikali inakiri kwamba, kuna matukio ya uhalifu yaliyotokea Zanzibar na Serikali inayafanyia kazi. Mhe. Mtolea alitaka kujua lipi ni jibu sahihi;

4. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi aliomba Mwongozo kuhusu kuzuiwa kupatikana kwa habari kupitia online TV hapa nchini. Alisema uzuiaji huo unanyima haki Wananchi kwani Wananchi wengi wanategemea kupata habari kutoka katika online TV. Hivyo aliomba mwongozo kwa nini utaratibu wa online TV usiendelee mpaka sheria ya kuzuia suala hilo itakapotungwa.

Mwenyekiti aliahidi kutoa majibu ya Miongozo hiyo wakati mwingine.

## VI. HOJA ZA KAMATI:

i. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mhe. Andrew John Chenge alisoma Taarifa ya Kamati na kutoa Hoja kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati yake pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hiyo;

ii. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mhe. George Huruma Mkuchika kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati yake pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hiyo;

iii. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mhe. Balozi Adadi Rajab alisoma Taarifa ya Kamati na kutoa Hoja kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati yake pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

Wabunge wafuatao walianza kuchangia:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Juliana Daniel Shoza | - | CCM |
| 2. | Mhe. Kanali Masoud Ali Khamis | - | CCM |
| 3. | Mhe. Mattar Ali Salum | - | CCM |
| 4. | Mhe. Mch.Peter Simon Msigwa | - | CHADEMA |

## VII. KUSITISHA SHUGHULI ZA BUNGE:

Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 Jioni.

## VIII. BUNGE KUREJEA:

Saa 10.00 Jioni Bunge lilirejea na Mhe. Najma Murtaza Giga (Mwenyekiti) aliongoza Bunge.

Wabunge wafuatao walichangia Hoja za Kamati:-

| | | |
|---|---|---|
| 5. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka | - | CCM |
| 6. Mhe. Cosato David Chumi | - | CCM |
| 7. Mhe. Jasson Samson Rweikiza | - | CCM |
| 8. Mhe. Anna Richard Lupembe | - | CCM |
| 9. Mhe. Hussein Mohammed Bashe | - | CCM |
| 10. Mhe. Zitto Zuberi Kabwe | - | ACT |
| 11. Mhe. Daniel Nsanzugwako | - | CCM |
| 12. Mhe. Joseph Roman Selasini | - | CHADEMA |
| 13. Mhe. Riziki Shahari Mngwali | - | CUF |
| 14. Mhe. Abdallah Ally Mtolea | - | CUF |
| 15. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi | - | CCM |
| 16. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete | - | CCM |
| 17. Mhe. Innocent Lugha Bilakatwe | - | CCM |
| 18. Mhe. Goodluck Asaph Mlingwa | - | CCM |
| 19. Mhe. Aida Joseph Khenani | - | CHADEMA |
| 20. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi | - | CHADEMA |
| 21. Mhe.Cecil David Mwambe | - | CHADEMA |
| 22. Mhe. David Ernest Silinde | - | CHADEMA |

### MWONGOZO WA SPIKA:

- Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliomba Mwongozo kuhusu ugawaji wa Madaraka kwa Wateule wa Rais, na kukanusha Maelezo kuwa Paul Makonda (RC Dar es salaam) anafanya kazi kama vile Makamu wa Rais na Waziri Mkuu yaliyotolewa na Mhe. David Silinde.

- Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe alitoa Taarifa kuhusu matukio yanayomuhusisha RC Paul Makonda na kujiinua kimadaraka ikiwa ni pamoja na tukio la kumuhusisha Waziri Mkuu na suala la Shisha, kauli yake kuwa kama angekuwa Waziri wa Uchukuzi asingeruhusu mambo yanayoendelea kufanyika hovyo katika sekta hiyo, na pia tukio lingine ni pale alipoonekana kumuamrisha Mheshimiwa Makamu wa Pili na kitendo chake cha kumzuia RAS wa Dar es salaam kufika kwenye kikao cha Kamati ya LAAC.

- Mheshimiwa Jenista Mhagama aliomba Mhe. Zitto na Mhe. Silinde waseme ni lini Mhe. Rais alimuapisha Makonda kuwa Waziri Mkuu au Makamu wa Rais. Na kwamba Mhe. Rais hajakasimu kazi za Viongozi hao kwa Mhe. Paul Makonda.

23. Mhe. Dkt. Suzan Kolimba

24. Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni
25. Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi
26. Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba

## IX. KUHITIMISHA HOJA ZA KAMATI:

1. Mhe. Andrew John Chenge , Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo alihitimisha Hoja ya Kamati yake kwa kujibu Hoja za Wabunge, Bunge lilihojiwa na kuyakubali Maoni na Mapendekezo ya Kamati hiyo;

2. Mhe. Capt. George Huruma Mkuchuka, Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge alihitimisha Hoja yake kwa kujibu hoja za Wabunge. Bunge lilihojiwa na kuyakubali Maoni na Mapendekezo ya Kamati hiyo;

3. Mhe. Balozi Adadi Rajab, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama alihitimisha Hoja yake kwa kujibu Hoja za Wabunge. Bunge lilihojiwa na kuyakubali Maoni na Mapendekezo ya Kamati hiyo.

   Mwenyekiti wa Bunge alitoka Kitini na kumpisha Spika, Mhe. Job Y. Ndugai ili aendelee na Shughuli zilizobaki kwa siku hiyo.

## X. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:

Katibu wa Bunge alitoa Taarifa kuhusu kukamilika kwa Shughuli zilizopangwa kufanyiwa kazi katika Mkutano wa Sita wa Bunge.

## XI. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:

- Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa alitoa Hotuba ya kuhitimisha Shughuli za Mkutano wa Sita wa Bunge, na kutoa Hoja ya kuahirisha Bunge hadi siku ya Jumanne tarehe 4 Aprili, 2017 Saa 3.00 Asubuhi;

- Spika aliwahoji Wabunge kuhusu Hoja ya kuahirisha Bunge na wote waliafiki. Aidha, Mhe. Spika aliwashukuru Wabunge wote na Viongozi wote wa Bunge kwa kuongoza Bunge Vizuri.

## XII. WIMBO WA TAIFA NA KUAHIRISHA BUNGE:

Saa 1.30 usiku Wimbo wa Taifa uliimbwa na Spika aliahirisha Bunge hadi siku ya Jumanne tarehe 4 Aprili, 2017 Saa 3.00 Asubuhi.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **DKT. T. D. KASHILILAH** |
| **10 FEBRUARI, 2017** | **KATIBU WA BUNGE** |